C. Kupeleka viwandani zitengeneza bidhaa mpya
D. Kuzichoma kwa moto

5. Yafuatayo ni mazingira ya shuleni ila

A. madarasa
B. misala
C. nyanja
D. misitu

6. Ni kipi hakitasababisha uchafuzi wa mazingira?

A. Upanzi wa miti
B. Utupaji plastiki
C. Kuelekeza uchafu mtoni
D. Kutotumia misala vyema

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 7 hadi la 12.

Zamani nyani na mbweha walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Waliishi pamoja na kufanya shughuli nyingi kwa ushirikiano, waliwinda wakalima na kufanya shughuli nyingi za nyumbani pamoja. Mara nyingine walifanya kazi zao kwa zamu.

Siku moja ilikuwa zamu ya nyani kwenda kuwinda. Alimwacha rafiki yake mbweha kuwalea wana na kutunza makazi yao mchana wote. Alijikaza kisabuni ili angalau wapate cha kutia mdomoni. Ilipofika jioni alikuwa amechuma matunda ya kutosha. Ama kweli atafutaye hachoki na akichoka keshapata. Alipofika nyumbani alimlaki kwa furaha tele. Walikula wakashiba wakasaza.

Mbweha kwa upande wake hakupenda kwenda kutafuta chakula alipenda kukaa nyumbani na kustarehe tu. Siku zilivyozidi kusonga alianza kuingiwa na mawazo maovu. Aliingiwa na tamaa na akaanza kugawa chakula walichoweka maghalani na kukipeleka kwingine. Kila mara akiba yao ilizidi kupungua. Nyani alipolalamika alimwambia kuwa wana wao wamekua na hivyo wanakula chakula kingi. Hata hivyo, ieleveke kuwa njia ya mwongo ni fupi. Nyani alianza kudadisi mambo na kutambua kuwa rafiki yake alikuwa akimhandaa. Alimfuata kisirisiri na kuona pale alipoficha chakula chao. Alimwendea mbweha na kumweleza mambo yote kinagaubaga. Mbweha alijawa na soni na kuahidi kubadilika. Nyani alikataa kuendelea na urafiki huo kwa kuwa alimwona rafikiye kuwa mnafiki na mwenye hila.

7. Chagua jibu linaloonyesha kuwa nyani na mbweha walikuwa na uhusiano mwema.

A. Walisaidiana kufanya mambo mengi
B. Walikuwa majirani waliotegemeana
C. Wangewinda pamoja
D. Walelezana mambo yote waziwazi.

8. Kwa mujibu wa kifungu, ni nani aliyefanya zamu ya kuwinda zaidi?

A. Mbweha na nyani
B. Nyani
C. Mbweha
D. Wana wao